**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**03** **MAARIFA YA JAMII**

**Muda: Saa 1:30** **MAJIBU** **Mwaka: 2018**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali manne (4).
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

SEHEMU A: (Alama 28)

1. Jibu kipengele cha (i) – (viii) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku.

i) Bibi na Bwana Juma wana mtoto aitwae Neema ambaye aliolewa na kuzaa mtoto aitwae Yusufu. Bwana Juma ni nani kwa Yusufu?

A. Baba

B. Babu

C. Mjomba

D. Mpwa

**B. Babu**

Bwana Juma ni baba wa Neema, naye Neema ni mama wa Yusufu. Hivyo Bwana Juma ni babu wa Yusufu.

ii) Ipi ni faida ya kiafya waipatayo wanafunzi kwa kucheza ngoma za kitamaduni?

A. Kuendeleza utamaduni.

B. Kupata hamasa ya kufanya kazi.

C. Kupata zawadi mbalimbali.

D. Kufanya mwili uwe imara na afya

**D. Kufanya mwili uwe imara na afya**

Ngoma za kitamaduni huhusisha harakati za mwili ambazo husaidia kuimarisha misuli na afya kwa ujumla.

iii) Bwana na Bibi James walioana mwaka 2014. Hawajafanikiwa kupata mtoto mpaka sasa. Hii familia inaitwaje?

A. Ya awali

B. Ya watoto yatima

C. Ya mke na mme

D. Ya makubaliano


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

**C. Ya mke na mme**

Familia yenye wanandoa bila watoto huitwa familia ya mke na mme.

iv) Kipi kati ya vifuatavyo ni kipaumbele cha Serikali ya awamu ya tano ya Tanzania?

A. Ubinafsishaji viwanda

B. Ujenzi wa viwanda

C. Elimu bure kwa Watanzania wote

D. Uanzishwaji wa vyama vingi vya siasa

**B. Ujenzi wa viwanda**

Serikali ya awamu ya tano ilijikita zaidi katika ujenzi wa viwanda kwa lengo la kukuza uchumi na ajira.

v) Ni kiongozi yupi katika Tanzania hupigiwa kura na wananchi kila baada ya miaka mitano?

A. Jaji Mkuu

B. Rais

C. Spika wa Bunge

D. Waziri Mkuu

**B. Rais**

Rais huchaguliwa moja kwa moja na wananchi kupitia uchaguzi wa kitaifa kila baada ya miaka mitano.

vi) Bwana John anamiliki mashamba makubwa ambayo huyakodisha kwa watu. Hii ni aina gani ya ukabaila?

A. Ubugabire

B. Ntemi

C. Nyarubanja

D. Ujima

**C. Nyarubanja**

Nyarubanja ni mfumo wa ukabaila ambapo mwenye ardhi hukodisha mashamba kwa watu wengine.

vii) Ni mawaziri wakuu wangapi waliofanya kazi katika serikali ya awamu ya kwanza ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

A. Wanne

B. Mmoja

C. Watatu

D. Wawili

**D. Wawili**

Katika awamu ya kwanza kulikuwa na Mawaziri Wakuu wawili waliotumikia serikali.

viii) Mfumo upi wa uzalishaji mali ulishamiri katika sehemu ya Magharibi mwa Tanzania?

A. Ujima

B. Ubugabire

C. Kihamba

D. Umwinyi

**B. Ubugabire**

Ubugabire ulikuwa mfumo wa uzalishaji mali uliotumika zaidi katika maeneo ya Magharibi mwa Tanzania.

2. Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha maeneo yenye madini mbalimbali katika Fungu A na aina za madini yanayopatikana katika Fungu B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

i) Geita mkoa wa Geita

**E. Dhahabu**


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

ii) Uvinza mkoa wa Kigoma

**G. Makaa ya mawe**

iii) Liganga mkoa wa Njombe

**D. Chuma**

iv) Mererani mkoa wa Manyara

**H. Tanzanite**

v) Karagwe mkoa wa Kagera

**B. Bati**

vi) Mwadui mkoa wa Shinyanga

**A. Almasi**

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu. Mazingira hujumuisha watu, miti, wanyama pamoja na vitu vingine. Kwa ujumla, mzaingira hujumuisha vitu vilivyo hai na visivy hai.

Mazingira ya shule huundwa na vitu vilivyo hai na visivyo hai. Mifano ya vitu vilivyo hai vinavyopatikana katika mazingira ya shule ni samani, vitabu, chaki, kalamu za wino, kalamu za risasi na vifutio vya ubao. Samani hujumuisha meza, dawati, viti na kabati. Vitu vyote vyenye uhai na visivyo na uhai vinavyopatikana katika mazingira ya shule yetu ni muhimu, hivyo tunapaswa kuvitunza

i) Kitu chochote kinachomzunguka binadamu huitwa

**mazingira**.

ii) Kipi kati ya mimea na samani ni kitu kisicho na uhai?

**Samani**.

iii) Mifano miwili ya vitu hai vinavyopatikana katika mazingira ya shule ni binadamu na

**miti**.

iv) Vitu visivyo hai ambavyo hupatikana katika mazingira ya shule ambavyo hutumika katika kuandikia na kuchorea ni kalamu ya wino, chaki na

**kalamu ya risasi**.

v) Kwa nini tunatunza vitu vilivyo hai na visivyo hai?

Tunavitunza **kwa sababu ni muhimu katika maisha na mazingira ya shule**.

vi) Kipi kati ya kabati na chaki ni mfano wa samani?

**Kabati**.

vii) Mbali na kundi la viumbe hai, kundi gani jingine linalopatikana katika mazingira ya shule?

**Vitu visivyo na uhai**.

4. Soma mchoro wa pande kuu nne za dunia uliopewa kisha jibu kipengele cha (i) – (iv) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

i) Kikombe kipo upande gani wa dira ya dunia?

Kikombe kipo **upande wa kusini**.

ii) Taja upande wa dunia wenye penseli.

Penseli ipo **upande wa kaskazini**.

iii) Kiti kipo upande gani wa dira ya dunia?

Kiti kipo **upande wa mashariki**.

iv) Upande wa dunia ambao jua linachomoza umewakilishwa na kitu gani?

Umewakilishwa na **kiti**, kwa kuwa jua huchomoza upande wa mashariki.



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***